# SKY FLYER EXAMINATIONS SERIES
## DARASA LA SITA
## MWAKA 2021

SKF21G

## KISWAHILI: LUGHA

**Muda: Saa 1 Dak. 40**

***SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI***

*1. Hakikisha umeandika*

*(i) Jina lako* *(ii) Jina la shule yako*

**Soma kifungu kifuatacho. Kwa nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi, umepewa manneno manne hapo chini. Changua neno lifaalo zaidi kati ya yale umpewa.**

Tangu ___1___ nimejiona___2___.Mema na mabaya.Mema ninayoburudikia___3___ mabaya ninayoyavumilia.Mtu hupata ajaliwalo wala sio___4___ .Ndoto yangu ___5___ nikiwa ___6___ ilikuwa kuwa mtangazaji___7___ runinga au ___8___. Nlijitahidi masomoni na kufanya mazoezi ya ___9___ kwa kufululiza.Niliweza hata kubadilisha sauti ___10___ kuwaiga___11___ ya watangazaji___12___. ___13___ kuwa nyota yangu ___14___ katika___15___bali katika ualimu.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | nilizaliwa | nilipozaliwa | nitazaliwa | nitakapozaliwa |
| 2. | wengi | mingi | mengi | kwingi |
| 3. | nayo | nalo | nacho | naye |
| 4. | atakacho | atakaye | atakayo | alitakalo |
| 5. | hadi | mpaka | tangu | kuliko |
| 6. | kidogo | mdogo | ndogo | wadogo |
| 7. | wa | la | kwa | cha |
| 8. | jarida | gazeti | rukono | redio |
| 9. | kuimba | kuruka | kuzungumza | kucheza |
| 10. | wala | ili | bali | lakini |
| 11. | Zaidi | licha | baada | baadhi |
| 12. | galacha | mbingwa | wahodari | wastadi |
| 13. | walijua | Tulijua | sikujua | mlijua |
| 14. | hazikuwa | halikuwa | hakukuwa | haikuwa |
| 15. | uchongaji | uanahabari | uchezaji | uigizaji |

**Kutoka swali la 16 - 30 jibu kulingana na maagizo uliyopewa**

16. Chagua sentensi iliyotumia **karibu** kuonyesha umbali wa wakati
   A. Ondoa karibu na moto
   B. Somo la kiswahili liko karibu kuanza
   C. Alikuwa mgonjwa karibu afe
   D. Njoo karibu nami

17. Andika kwa wingi:
   shati lake limechafuka
   A. Shati zao zimechafuka
   B. Mashati zetu zimechafuka
   C. Mashiti yetu yamechafuka
   D. Mashati yao yamechafuka

18. Mstari mmoja katika ushairi huitwaje?
A. ubeti
B. mshororo
C. kina
D. kibwagizo

19. Chagua sentensi iliyotumia kirenjeshi <u>ndi</u> kwa usahihi
A. mimi ndite mwalimu wenu
B. yeye ndiyo aliyenisaidia
C. Sisi ndio tulioshinda
D. nyiny ndinyi washidi wa leo


20. Mshindi alipoenda kumzuru nyanya yake jioni, alimsalimia;
A. hujambo?
B. sabalkheri
C. masalkheri
D. shikamoo

21. Sare ya wanajeshi huitwa?
A. jezi
B. surupwenye
C. kasula
D. kombati

22. Chagua sentensi iliyoakifishwa barabara
A. kifaduro;ni ugonjwa mbaya
B. Je?unaenda wapi?
C. Lo!Amefeli mtihani!
D. Tutaonana kesho asubuhi

23. Nomino dhahania inayoundwa na kitenzi penda ni:
A. upendo
B. Mapenzi
C.Kupenda
D. Pendeza

24. Umbo hii huitwa?



A. Mche
B.duara
C.Pia
D.Pembe tatu

25. Vazi la Kike linalofanana na shati ni
A.Kanchiri
B.bwelasuti
C.blauzi
D.kaptura

26. Andika kwa wingi
Kikombe changu kimpa suka
A.vikombe vyangu vimepasuka
B.Vikombe vyetu vimepasuka
C.vikombe zetu zimepasuka
D.vikombe vyangu vimepasuka

27. Mtoto aliyefiwa na wazazi ni
A.Mjane
B.Malaika
C.Fukara
D.Yatima

28. Changanua kiunganishi sahihi kujaza pengo. Ndirangu ni mzuri darasani __________hupenda kuchelewa.
A.kwa sababu
B.la sivyo
C.fauka ya
D.Ispokuwa

29. Kanusha , Nafanya mtihani
A.Twafanya mitihani
B.Nafanya marudio
C.Sifanyi marudio
D.Sifanyi mtihani

30. Taja methali yenye maana sawa na:-
Nazi mboni harabu ya nzima
A.Pole pole ndio mwendo
B.Kidole kimoja hakivunji chawa
C.Nzi mmoja huoza nyama
D.Maji yakimwangika hayazoleki

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu mawali 31-40**

Wakonyo alikuwa msichana wa umri wa mwongo mmoja.Alizaliwa na wazazi wakwasi. Chochote alichokihitaji alikipata kwa wakati uliofaa. Hakujua maana ya neno shida.Hata hivyo,Wakonyo alikuwa na dosari moja -upuuzaji chochote alichoambiwa, alipuuzilia mbali.Wazazi na walimu walimwonya dhidi ya hulka hii lakini aliyotia masikio komango . Ama kweli, sikio la kufa halisiki______________.

Siku moja, Wakonyo alionywa dhidi ya kuzungumzia watu asiyowajua lakini kama kawaida aliwaona wazazi wake kama wenye maonyo mengi tu."Kwani kuna ubaya gani kuongea na watu ?"Akajiuliza alipotokea shuleni jua lilipokuwa likibusu milima ya magharibi,alikutana na watu watatu .Walimsalimia kisha wakaanza kumuuliza kama alikuwa anajua chifu wa kata hiyo.Aliwambia kwamba Chifu alikuwa baba yake. Wanaume hao walimwambia aingie kwenye gari lao awapeleke kwake chifu kwani walikuwa na ujumbe wake.

Pasi na kuwaza,Wakonyo alijituma ndani ya gari lao awpeleke ndani ya gari lao na punde tu alipoketi, alizibwa pua kwa kitambaa chenye unyevu.Kutoka hapo,Wakonyo akona giza.Alipopata fahamu, alijikuta amefungwa mikono na miguu,katika nyumba moja ambayo hakuifahamu.Papo hapo, akakumbuka maneno aliyoambiwa na walimu na wazazi kuhusu kutopuuza.Alitaka kurekebisha aanza kutii lakini tayari alikuwa amechelewa kwani tayari alikuwa amenaswa.

Alilia kwa uchungu lakini hakujua majuto ni mjukuu huja baadaye.

31. Wakonyo alikuwa na umri wa miaka mingapi?
A.Tisa
B.Kumi
C.Kumi na moja
D.Mitano

32. Wazazi wa Wakonyo walikuwa matajiri kwa nini
A.Walikuwa wakwasi
B.Walipata chochote walichotaka
C.Walimpa mwanao alichohitaji
D.Walikuwa na shinda nyingi.

33. Wakonyo alikuwa na kasoro gani?
A.Kupuuza
B.Shinda
C.Kujuta
D.Kuongea sana

34. Wakonyo alionywa dhidi ya kufanya nini?
A.kuzungumza na watu
B.Kupuuza aliyoambiwa
C.Kuyatia masikio komango
D.Kuwazungumzia watu asiyowajua.

35. Kulingana na aya ya kwanza, methali iliyotumiwa ingekamilishwa aje?
Sikio la kufa halisikii________________
A.Matibabu
B.Dawa
C.Kafara
D.Daktari

36. Watu aliokutana na Wakonyo walikuwa wakitaka?
A.Kuzungumza na Wakonyo
B.Kujua alikoishi Chifu
C.Kumteka Wanyoro nyara
D.Kumpelekea chifu ujumbe.

37. Wakati Wakonyo alipopata fahamu,
A.Alijikuta hospitalini
B.Alijipata nyumbani kwao
C.Alijipata amezibwa
D.Alijipata asikojua akiwa amefungwa mikono na miguu.

38. Baba Wakonyo alikuwa
A.Maskini saha
B.Chifu wa kata walioishi wakonyo
C.Mwalimu mkuu wa shule aliyosoma Wakonyo
D.Mchungaji wa kanisa aliloshiriki Wakonyo

39. Tukio lilompata Wakonyo lilimfanya_____
A.Abadilishe tabia
B.Awe mtundu zaidi
C.Awaelekeze wageni
D.Aingie ndani ya gari la watu asiojua

40. Wakonyo alitoka shuleni wakati gari?
A.Adhuhuri
B.Asubuhi
C.Jioni
D.Alasiri

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41-50**

Baada ya Uhuru, Kenya ilihitaji kuikweza lugha moja ya kiasili kuwa lugha ya taifa.Wakenya hawakutaka kuitumia lugha ya taifa.Hii ilionekana kuwa lugha ya kikoloni na kigeni. Hali ya kuwepo lugha nyingi ndiyo ilitatiza uchanguzi wa lugha moja .Kila kabila lilitarajia lugha yake kuchanguliwa ,jambo ambalo lilikuwa gumu, kuchangua kingereza hakunge faa kwani, mbali na wasomi raia wengi hawakukijua.Hata sasa, Wanainchi wengi bado hawajakimudu.

Serikali ilishughulikia swala hili la uteuzi.**Hatemaye** kiswahili kilitunukiwa hadhi ya kuchanguliwa kama lugha ya taifa.Kiswahili hutumika katika maongezi ya kawaida, mawasiliano ya kibiashara na kadhalika.Kiswahili kilichaguliwa kwa sababu kadhaa. Kwanza baadhi ya wasomi walifikiri kwamba lugha hii kuwa na asili ya kiarabu. Kwa sababu hii, walifikiria kuwa kiswahili hakikuwa lugha ya kabila lolote.

Pili wengine waliamini kwamba kiswahili ni mchanganyiko wa lugha ya kiarabu na lugha ya kiafrika. Kingekubaliwa na makabila yote.Hata hivyo, wasomi wengine hawasikilii kuwa hii ilikuwa ni lugha ya kiafrika asilia bila mchanganyiko wowote.Hivi leo **hakuna ubishi wowote** kuhusu asili ya kiswahili. Hii ina maana kuwa Kiswahil kimekubalika kama lugha ya kiasili afrika mashriki.Pia ni kitambulisho cha Utaifa wa nchi kama Kenya na Tanzania.Isitoshe kiswahili ni lugha mojawapo ya lugha za taifa nchini Congo, Rwanda na Burundi.

41. Ni nini hasa kilichotatiza uchaguzi wa lugha ya taifa?
A.Wakenya walijua lugha nyingi tofauti
B.Hakukuwa na lugha nyingi tofauti
C.Hakukuwa na lugha nyingi nchini kenya
D.Wakenya hawakutaka kuchagua lugha ya kikoloni

42. Kwa nini haingefaa kuchagua kiingereza?
A.Ilikuwa ya wasomi na raia
B.Ilionekana lugha ngumu isiyoweza kueleweka.
C.Si watu wengi walioweza kukiongea
D.Wenyeji walichukia wageni na lugha yao

43. Kulingana na taarifa, Lugha ya taifa hutumika vipi nchini Kenya?
A.Katika mawasiliano ya siasa na shughuli rasmi
B.Katika mawasiliano ya kawaida, biashara, siasa na dini
C.Katika maongazi ya kawaida na dini
D.Katika maongazi za mawasiliano ya serekali

44. Kwa nini Kiswahili hatimaye kilichaguliwa kuwa lugha ya taifa
A.Uamuzi huo ulitolewa na wasomi
B.Kilikiriwa tu kuwa ni lugha ya kiarabu
C.Kilitumika kwingi barani Afrika
D.Kwa sababu kilifikiriwa kuwa si lugha ya kundi lolote

45. Maana ya neno **hatimaye** ni?
A.Baadaye
B.Aghalabu
C.Tena
D.Mwanzoni

46 Uliposoma habari hii, ulipta jumla ya maoni mangapi juu ya asili ya kiswahili?
A.mawili
B.moja
C.matatu
D.Manne

47 Maana ya neno hadhi kama ilivyotumika katika kifungu ni
A.Heshima
B.Zawadi
C.Umaarufu
D.Ubora

48. Lugha ya taifa nchini ni muhimu kwa kuwa
A.Hutumika kwa watu wengi
B.Huimarisha amani na nchi jirani
C.Ni kitambulisho cha utaifa
D.Hupendwa na watu wengi

49. Maana ya **hakuna ubishi wowote** ni
A.Jambo la kujadiliana
B.Hakuna pingamizi zozote
C.Jambo lisilo wazi
D.Hakuna kunafikiana tena

50. "Kiswahili ni lugha moja wapo ya lugha za taifa." Hii inamaanisha?
A.Ni lugha ya kimataifa
B.Ni lugha ya kiasili
C.Kuna lugha zingine za taifa
D.Ndiyo lugha pekee ya taifa